**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**
**CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION**

**015/2**

# ELIMU YA DINI YA KIISLAMU 2

(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)

**Muda: Saa 2:30** **Alhamisi, 10 Novemba 2016 mchana**

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C na D.
2. Jibu maswali **manne (4),** swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama 25.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.


KM-2016

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

**BISMILLAHIR - RAHMANIR - RAHIM**

## SEHEMU A: QUR'AN

1. Uthibitisho kuwa Qur'an ni neno la Allah (s.w) ni pamoja na:
   (a) Kutokea kweli matukio yaliyotabiriwa katika Qur'an.
   (b) Kukosolewa Mtume (s.a.w) ndani ya Qur'an.
   Thibitisha madai haya kwa kutumia ushahidi wa matukio manne kutoka kipengele (a) na matukio mawili kutoka kipengele (b).

2. Andika tafsiri ya Surat Lahab (111:1-5) kisha eleza mafunzo manne yatokanayo na Sura hiyo.

3. *"Hiki ni kitabu kisichokuwa na shaka ndani yake, ni uongozi kwa wamchao Mwenyezi Mungu"* (2:2). Kwa kuzingatia aya hii, toa hoja tano za kuwashauri Waislamu cha kufanya ili waongozwe na Qur'an.

## SEHEMU B: TAWHIID

4. Katika historia ya mwanadamu hadi kufikia leo hii, Allah (s.w) amekuwa akishirikishwa katika nyanja tofauti. Jadili usemi huu kwa kuchambua matapo manne ya shirki na namna yalivyoenea katika jamii.

5. *"Katika kuumbwa mbingu na ardhi na mfuatano wa usiku na mchana ziko alama (hoja za kuonesha kuwepo kwa Allah (s.w) kwa wenye akili"* (3:190). Kwa kuzingatia aya hii, chambua alama sita zilizomo mbinguni na ardhini zinazothibitisha kuwepo kwa Allah (s.w).

6. Kwa kutumia hoja sita, fafanua ushahidi wa kihistoria ndani ya Qur'an unaothibitisha kuwa ufufuo ni jambo jepesi kwa Allah (s.w).

## SEHEMU C: FIQHI

7. Toa maana pana ya nguzo ya kwanza ya Uislamu na kisha onesha umuhimu wa nguzo hiyo kudhihirishwa katika namna tatu.

8. Ukiwa kama imamu katika msikiti, wafahamishe maamuma wako namna wanavyotakiwa kumswalia maiti.

9. Kwa kutumia hoja sita, tathmini namna utimizaji wa masharti ya kutoa Zakat unavyosababisha kufikiwa lengo la nguzo hii ya Uislamu katika jamii.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner

## SEHEMU D: TAREKH

10. Fafanua mafunzo sita yatokanayo na historia ya maisha ya Muhammad (s.a.w) kabla ya kupewa utume.

11. *"Bila shaka tumekwisha kupa kushinda kuliko Dhahiri"* (48:1). Kwa kuzingatia aya hii, ainisha matokeo manane yanayodhihirisha ushindi wa Waislamu kupitia mkataba wa Hudaibiya.

12. Eleza mbinu sita alizotumia Nabii Ibrahim (a.s) katika kulingania watu wake.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org
Scanned by CamScanner